TANGAZO LA SERIKALI Na. 717 la tarehe 6/10/2023

SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA,
(SURA YA 191)

# KANUNI

*(Zimetengezwa chini ya kanuni ya 230(2)(i))*

MAREKEBISHO YA KANUNI ZA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (USIMAMIZI NA UDHIBITI WA KEMIKALI ZINAZOMONG'ONYOA TABAKA LA OZONI NA HIDROFLUOROKABONI) ZA MWAKA 2023

Jina

TS. Na. 582 la 2022.

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Udhibiti wa Usimamizi wa Kemikali zinazomongónyoa Tabaka la Ozoni) za mwaka 2023, na zitasomwa pamoja na Kanuni za Usimamizi wa Mazingira (Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni na Hidrofluorokaboni) za Mwaka 2022, ikirejewa kama "Kanuni kuu"

Marekebisho ya kanuni ya 27

2. Kanuni kuu inarekebishwa katika kanuni ya 27, kwa kuongeza maneno "kwa kutumia vifaa maalum" baada ya maneno "kemikali zinazodhibitiwa" yanayoonekana katika aya ya (b).

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

3. Kanuni kuu inarekebishwa katika aya ya 1 ya Jedwali la Kwanza kwa kuongeza neno "viyoyozi vya" kabla ya neno "magari".

Marekebisho ya Jedwali la Nne

4. Kanuni kuu inarekebishwa katika Jedwali la Nne kwa kuondoa maneno "kanuni ya 20(2)" yanayoonekana katika kifungu wezeshi.

Dodoma,
21 Septemba, 2023

SELEMANI SAIDI JAFO,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira*